

## TAARIFA KWA UMMA



### WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT KWA KUJITOLEA MWAKA 2022

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, anatoa wito kwa Vijana wote wa Tanzania Bara na Visiwani kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujitolea kwa mwaka 2022.

Utaratibu wa Vijana kuomba na hatimaye kuchaguliwa kujiunga na mafunzo hayo, unaratibiwa na Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambako mwombaji anaishi.

Utaratibu wa maandalizi ya Vijana hao kwaajili ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujitolea unaanza leo hii tarehe 25 Agosti 2022. Vijana watakaoteuliwa wanatakiwa kuripoti kwenye Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa mwezi Septemba 2022.

Aidha, Jeshi la Kujenga Taifa linapenda kuwataarifu Vijana watakaopata fursa hiyo kuwa **halitoi ajira** kwa vijana, Pia halihusiki kuwatafutia Vijana ajira katika Asasi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Mashirika mbalimbali ya Serikali na yasiyo ya Kiserikali, Bali hutoa mafunzo ambayo yatawasaidia Vijana kujajiri wenyewe mara baada ya kumaliza Mkataba wao na Jeshi la Kujenga Taifa

Sifa za Muombaji ni kama ifuatavyo:-


1. Awe Raia wa Tanzania
2. Elimu na Umri
  - a. Kwa Vijana wenye elimu ya Darasa la Saba, umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18.
  - b. Vijana wenye elimu ya Kidato cha Nne, umri usiwe zaidi ya miaka 20
  - c. Vijana wenye elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe chini ya miaka 18 na usiwe zaidi ya miaka 22.
  - d. Vijana wenye elimu ya Stashahada umri usizidi miaka 25.
  - e. Vijana wenye elimu ya Shahada, umri usiwe zaidi ya miaka 26.
  - f. Vijana wenye elimu ya Shahada ya Uzamili, umri usiwe zaidi ya miaka 30.
  - g. Vijana wenye elimu ya Shahada ya Uzamivu, umri usizidi miaka 35.
3. Awe na afya njema, Akili timamu na asiwe na alama yoyote ya mchoro mwilini (Tattoo)
4. Mwenye Tabia na Nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.

5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari kidato cha Nne na sita wawe waliomaliza kuanzia mwaka 2019, 2020, 2021 na 2022 wenye ufaulu ufuatao:-
  - a. Vijana kidato cha nne Wawe na ufaulu wa alama zisizopungua 32
  - b. Vijana kidato cha Sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne
6. Awe na elimu ya msingi aliyehitimu darasa la saba
7. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate)
8. Awe na cheti halisi cha kumaliza shule (School Leaving Certificate)
9. Awe na cheti Halisi cha Matokeo (Original Academic Certificate /Transcript)
10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au KMKM wala Kuajirwa na idara nyingine za Serikalini.
11. Asiwe amepitia JKT katika operesheni za nyuma.
12. Asiwe amejihushisha na matumizi ya dawa za kulevya, bangi au yanayofanana na hayo.
13. Kwa wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na Sanaa, sifa za elimu ni sawa na zilizotajwa hapo juu.

JKT linawataka vijana watakaochaguliwa kuripoti makambini wakiwa na vifaa vifuatavyo:-

1. Bukta ya rangi 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni (elastic) iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini isiyo na zipu.
2. Raba za michezo zenye rangi ya kijani au blue.
3. Shuka mbili za kulalia zenye rangi ya blue bahari.
4. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
5. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi.
6. Truck suit ya rangi ya kijani au blue.
7. Flana ya kijani kibichi yenye kola ya duara isiyo na maandishi.

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele anawaalika Vijana wote watakaopata fursa hiyo kuja kujifunza Uzalendo, Ukakamavu, Stadi za Kazi, na Stadi za Maisha na pia kuwa tayari kulilinda na kulitumikia Taifa letu.



**Imetolewa na:**  
**Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,**  
**Makao Makuu ya JKT,**  
**Tarehe 25 Agosti 2022.**